## Benki ya Ushirika kuwapa elimu ya fedha wakulima wa korosho Kusini

**Na Sijawa Omary, Tandahimba**

BENKI ya Ushirika Tanzania (CBT), Tawi la Tandahimba mkoani Mtwara imepanga kuwanoa wakulima wa mazao mbalimbali ikiwemo la korosho katika mikoa ya kusini kuhusu elimu ya fedha ili kuhakikisha wanatumia huduma hizo kwa manufaa yao na kuepukana na madeni yasiyolipika.

Akizungumza mkoani Mtwara wakati wa uzinduzi wa huduma za benki hiyo, Meneja wa Benki ya Ushirika wa tawi hilo la Tandahimba, Baraka Ondiek alisema wanatambua mchango mkubwa wa wakulima katika uchumi wa taifa hasa kwenye ukanda huo wa kusini unaojulikana kwa uzalishaji wa korosho.

Uzinduzi wa huduma hizo za kibenki umefanyika katika Kijiji cha Mnyawa kilichopo wilayani humo na itahudumia wakulima katika mkoa huo wa Mtwara, Lindi pamoja na Ruvuma.

"Ujio wa benki hii ni suluhisho la changamoto za kifedha zinazowakabili wakulima wa mikoa hii, lengo kuu ni kuwawezesha wakulima kupata mikopo kwa riba nafuu, kuweka akiba kwa usalama na kusimamia fedha zao kwa ufanisi zaidi," alieleza.

"Tunatambua mchango mkubwa wa wakulima katika uchumi wa taifa, hasa katika ukanda huu wa Kusini unaojulikana kwa uzalishaji wa korosho. Benki yetu imekuja kuwapa suluhisho la kifedha kwa kuwapa mikopo rafiki na huduma za kibenki zinazokidhi mahitaji yao," alisema Ondiek. Aliongeza: "Benki hii pia itaendelea kutoa elimu ya kifedha kwa wakulima hawa ili kuhakikisha wanatumia huduma hizi kwa manufaa yao zaidi na kuepukana na changamoto za madeni yasiyolipika".

Alisema benki hiyo inatarajiwa kuwa nguzo muhimu kwa maendeleo ya sekta ya kilimo kusini mwa Tanzania hasa kwa kusaidia wakulima wadogo na wa kati kupata mitaji na huduma za kifedha kwa urahisi zaidi.

Baadhi ya wakulima wa zao hilo la korosho waliohudhuria hafla hiyo akiwemo mkazi wa kijijini hapo, Hamisi Juma alieleza moja ya matumaini yao watakayopata kupitia benki hiyo, ni pamoja na kuwarahisishia upatikanaji wa mikopo kwa riba nafuu, hivyo kuwa mkombozi kwao.

# Wakulima wa tumbaku Ru… washauriwa kuzalisha kwa…

**Na Muhidin Amri, Songea**

MENEJA Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Songea na Namtumbo mkoani Ruvuma (SONAMCU), Juma Mwanga amewataka wakulima wa tumbaku kuongeza uzalishaji wa zao hilo ili wajipatie kipato kikubwa na kuondokana na umaskini.

Mwanga alitoa wito huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari walipotembelea shamba darasa lililopo katika Kata ya Mletele, Manispaa ya Songea na kujionea ubora wa shamba hilo la tumbaku lenye ukubwa wa ekari 25 pamoja na shughuli zinazofanywa ikiwemo upuliziaji wa dawa.

Alisema ndani ya miaka minne zao la tumbaku lilikuwa linayumbayumba na changamoto kubwa ilikuwa soko la uhakika na mazingira wezeshi ya wanunuzi wa tumbaku nchini hasa baada ya kampuni nyingi kuondoka.

"Kuna kampuni nyingi zimekuja kununua tumbaku Tanzania kwa mfano wa uzalishaji wa mwaka jana hapa nchini ulikuwa zaidi ya tani 144,000 na zote zilinunuliwa ukilinganisha na tani 37,000 kwa mwaka 2020 zilizouzwa nje ya nchi," alisema Mwanga.

Alisema mwaka jana zao la tumbaku limeongezeka kutoka tani 67,000 kwa mwaka 2023 mpaka tani 144,000 na matarajio ya msimu wa kilimo 2025/2025 kuzalisha tani zaidi ya 300,000. Akizungumzia kuhusu kiwanda cha kusindika Tumbaku cha Sontop kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambacho kwa muda mrefu hakifanyi kazi, alisema kiwanda hicho kimek… kuwa mdog… kwa mwaka… tumbaku ta… wa miaka m… tani 1,000.

"Kwa hi… cha Ushirika… kiwanda ki… lazima kuta… kwa takriba… ili uzalishaji… anza kufikir… alisema.

## Tume kukagua haki za binadamu viwandani Pwani

**Na John Gagarini, Kibaha**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imeanza ziara kutembelea viwanda mkoani Pwani ili kuangalia uzingatiwaji wa haki za binadamu ili zisivunjwe.

Hayo yalisemwa Mjini Kibaha na Kamishna wa Tume, Nyanda Shuli wakati wa ziara ya kutembelea viwanda juzi ili kufanya uchunguzi kujua kama kuna changamoto za uvunjifu wa haki za binadamu.

Shuli alisema kuna baadhi ya viwanda vimekuwa vikilalamikiwa na wananchi na wafanyakazi kuwa vinavunja haki za binadamu kwa unyanyasaji wa wafanyakazi, uchafuzi taka maji na haki mbalimbali.

"Lengo la ziara ni kuangalia iwapo haki za binadamu zinazingatiwa, kuangalia usalama wa mazingira ya kazi na uzingatiaji wa viwango vya ajira," alisema.

Shuli alisema malalamiko waliyoyapokea watayafanyia kazi na kutoa majibu, jambo kubwa ni kuona haki inatendeka ili kuondokana na uvunjifu wa haki za binadamu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kiwanda cha Keds Tanzania kinachojihusisha na uzalishaji wa sabuni za unga na vipande, maji, pampasi na taulo za kike, Bob Chen alisema kiwanda hicho kinazingatia haki za wafanyakazi na wananchi wanaozunguka kiwanda.

Chen alisema kiwanda chao lengo lake ni kukuza uchumi wa wananchi na hata maji ya kiwanda hicho hayana madhara ambapo asilimia 60 ya wafanyakazi wanaishi eneo jirani na kiwanda, hivyo kama kungekuwa na changamoto hata wao wangeipata.

Alisema wanafanya utafiti ili kuongeza bidhaa na uzalishaji wenye kuzingatia ubora na bei ambayo inaendana na soko ambalo liko nchi nzima na baadhi ya nchi ikiwa ni pamoja na Kenya, Uganda na Malawi na sehemu nyingine.


